Mbolea Inachangia Katika Ukuaji wa Wakulima, Chakula, na Mapato

Imeandikwa na Busani Bafana

Wakulima wadogo wadogo watafanikiwa ikiwa wanaweza kupata maarifa na matumizi ya pembejeo za kilimo kama vile mbolea na mikopo. Picha ni kwa hisani ya: Busani Bafana / IPS

Louis Trichardt, Afrika Kusini, Julai 26, 2016 (IPS) – Unapoingia katika duka la muuzaji za bidhaa za kilimo Bi. Nancy Khorommbi, lilo kwenye kona ya kituo cha huduma za magari, mifuko ya mbolea na pakiti za kila aina ya mbegu zinavutia macho yako.

Lakini mbegu na mbolea anazouza hazijakuwa zikinunuliwa kwa kasi tangu Khorommbi alipofungua duka lake miaka sita iliyopita. Wateja wake: ambao ni wakulima wadogo wadogo katika mji mdogo wa Sibasa, kilomita 72 kaskazini mashariki mwa Louis Trichardt katika mkoa wa Limpopo, mojawapo ya mikoa ya Afrika Kusini ambayo imeathirika vibaya na ukame mwaka huu. Sababu ya kuwepo kwa biashara duni ni kwamba wakulima wadogo wadogo hawawezi kupata, na pia hawawezi kutumia mbolea ya kunawirisha mimea ifaavyo ili kuboresha uzalishaji wao wa chini katika kilimo.

"Baadhi ya wakulima ambao huja dukani mwangu hawajawahi kusikia kuhusu mbolea na wakulima wale ambao wamesikia kuhusu mbolea, hawajui jinsi ya kutumia mbolea kwa njia sahihi," Khorommbi aliambia IPS wakati wa warsha ya mafunzo iliyoandaliwa na Shirika la Kimataifa la Mbolea (International Fertilizer Association -IFA) kwa ushirikiano na Programu wa Wadhamini wa Mbolea Barani Afrika (African Fertilizer Volunteers Program-AFVP) ili kuwafundisha wakulima wadogo wadogo na wafanyabiashara wa bidhaa za kilimo kama Khorommbi kuhusu mbolea mjini Limpopo.

Khorommbi anayefafanua kuwa elimu ni nguvu, anaeleza kwamba uendelezaji wa biashara za wafanyabiashara wa bidhaa za kilimo ni kiungo muhimu katika mfumo wa uzalishaji wa chakula. Wafanyabiashara wa bidhaa za kilimo, ambao wanafanya kazi vijijini, wanaelewa vyema zaidi na wanaweza kuwapata wakulima wadogo wadogo kwa

urahisi. Wakulima ambao mara nyingi huenda wanategemea huduma duni za kilimo za serikali ambazo hazifadhiliwi vyema ili kupata maelezo kuhusu uboreshaji wa kilimo chao.

"Wakulima wadogo wadogo wanaweza kuleta mabadiliko katika usalama wa chakula kupitia uboreshaji wa kilimo chao, mojawapo ya kipengele muhimu katika uboreshaji huu ni matumizi ya mbolea," Khrorommbi ambaye ni mmoja ya wafanyabiashara 100 wa bidhaa za kilimo katika wilaya ya Vhembe, mkoa wa Limpopo alisema.

Msaidizi wa Khorommbi anaangalia bidhaa zilizopo katika duka la Nancy Khorommbi la bidhaa za kilimo wilayani Vhembe, Mkoa wa Limpopo, Afrika Kusini. Picha ni kwa hisani ya: Busani Bafana / IPS

Kuongezeka kwa maarifa, ni kuwakuza wakulima

Shirika la Ushirikiano wa Mbolea na Kilimobiashara Barani Afrika (African Fertilizer and Agribusiness Partnerships - AFAP), likibainisha pengo la maarifa lililopo ambalo liliungwa mkono na Shirika la Umoja wa Mataifa la Chakula na Kilimo (FAO) na washirika wa sekta ya kibinafsi, lilizindua Mradi wa Usaidizi wa Kilimobiashara katika Mkoa wa Limpopo (Agribusiness Support to the Limpopo Province -ASLAP) katika mwaka wa 2015, mradi ambao umewapa mafunzo wafanyabiashara wa bidhaa za kilimo zaidi ya 100 katika mkoa wa Limpopo.

Mradi huu unalenga kuchukua muundo wa kukuza kitovu cha wafanyabiashara wa bidhaa za kilimo, ambapo biashara kubwa za bidhaa za kilimo zinatoa bidhaa kwa wafanyabiashara wa bidhaa za kilimo wadogo wadogo na maajenti katika maeneo ya mashambani; maajenti hawa hatimaye watatoa huduma bora kwa wakulima wadogo wadogo kwa kuhakikisha kuwa pembejeo za kilimo zinaweza kupatikana na wakulima kwa urahisi na kwa bei nafuu. Programu ya Wadhamini wa Mbolea Barani Afrika (AFVP) inalenga kuvuta sekta ya kibinafsi nchini Afrika Kusini - mtandao wa wauzaji wa mbolea- ili kuimarisha sekta ya Wajasiriamali wadogo na wa kati (SME) katika mtandao wa usambazaji wa mbolea huku ikilenga wakulima wadogo wadogo na wafanyabiashara wa bidhaa za kilimo.

Wakulima wadogo wadogo ndio wanalilisha bara la Afrika, ikiwa ni pamoja na nchi ya Afrika Kusini, lakini uzalishaji wao umedunishwa na uwezo wao duni wa kupata pembejeo na hata masoko ya kununua bidhaa zao, suala ambalo Shirika la Umoja wa Mataifa la Chakula na Kilimo (FAO) linaamini kwamba ushirikiano baina ya sekta ya umma na kibinafsi unaweza kulitatua.

Katika harakati za kupunguza “pengo la mazao ya kilimo” lililopo miongoni mwa wafanyabiashara wadogo wadogo, Shirika la Afrika la Mbolea na Kilimobiashara (AFAP) likishirikiana na kampuni ya kibinafsi, ya Mbolea ya Kynoch (Kynoch Fertilizer), wameanzisha mradi wa ukuzaji wa ujasiriamali unaolenga wakulima wadogo wadogo na wafanyabiashara wa bidhaa za kilimo katika mkoa wa Limpopo, mojawapo ya eneo kuu la kilimo nchini. Wakulima wadogo wadogo na wafanyabiashara wa bidhaa za kilimo wamepewa mafunzo kuhusu, udongo, virutubishi vya mimea, uhifadhi salama wa mbolea, usalama wa mazingira na ujuzi wa usimamizi wa biashara.

"Kwa kutumia mbolea kwa njia sahihi zaidi, wakulima wadogo wadogoo wa Afrika Kusini wanaweza kukuza chakula chenye lishe bora zaidi, huku wakiafikia usalama wa chakula nyumbani mwao, hatimaye watabuni nafasi zaidi za ajira na kukuza maendeleo katika maeneo ya mashambani, Prof. Richard Mkandawire, ambaye ni rais wa Shirika la Afrika la Mbolea na Kilimobiashara (AFAP) aliambia IPS. "Kukuza na kuunga mkono sekta ya Wajasiriamali wadogo na wa kati (SME) barani Afrika ndio njia ya kuchukua ikiwa tunataka kupunguza njaa na umaskini. Maisha ya siku zijazo ya Afrika Kusini yanahusu ukuaji wa biashara za maeneo ya mashambani ambao utasaidia wakulima wadogo wadogo na kuongeza nafasi za ajira.'

Mnamo mwaka wa 2006, Wakuu wa Nchi za Afrika na Serikali walitia sahihi kwenye Azimio la Abuja katika Mkutano wa Kimataifa kuhusu Mbolea uliofanyika nchini Nigeria. Walijitolea kuongeza matumizi ya mbolea barani Afrika kutoka kiwango cha wastani cha wakati huo cha Kilogramu 8 kwa kila hekta hadi Kilogramu 50 kwa kila hekta kufikia mwaka wa 2015 ili kukuza uzalishaji wa wakulima. Miaka kumi baadaye, ni nchi chache pekee ambazo zimeweza kuafikia lengo hili.

Mkandawire alifafanua kuwa utafiti umeonyesha kwamba kwa kila kilogramu ya virutubishi wakulima wadogo wadogo wanatumia kwenye udongo wao, wanaweza kuongeza mazao yao na hadi kilogramu 30 zaidi.

Utafiti umeonyesha kwamba wakulima wadogo wadogo nchini Afrika Kusini kwa ujumla hawatumii viwango vya juu vya mbolea kutokana na gharama kubwa, uwezo duni wa kupata mbolea na ufahamu mdogo kuhusu manufaa ya kuweka virutubishi kwenye udongo ambao unaotumiwa na wakulima kwa kilimo chao.

Msajili na Mkurugenzi wa Mbolea katika Idara ya Kilimo, Uvuvi na Misitu (DAFF) katika mkoa wa Limpopo Jonathan Mudzunga anasema kuwa wakulima wadogo wadogo wana matatizo ya kupata mbolea ambayo wanaihitaji zaidi. Mbolea ni pembejeo muhimu katika kuongeza mazao ya kilimo na kutoa fursa za biashara na ajira kwa wafanyabiashara wa bidhaa za kilimo.

"Wakulima wakubwa wanaouza mazao yao wamefanikiwa kwa sababu wanaweza kupata mbolea na pembejeo kama vile mbolea na maarifa ya kuitumia. Hili halimaanishi kwamba wakulima wadogo wadogo wanapata changamoto kwa sababu hawajui jinsi ya kufanya kilimo lakini suala kubwa mno ni ukosefu wa maarifa na uwezo wa kupata pembejeo," Mudzunga alisema.

Mwanakilimo katika Kynoch, Schalk Grobbelaar, anasema kuwa uzalishaji wa mazao ya kilimo wa wakulima wadogo wadogo mkoani Limpopo unazuiliwa na matumizi madogo ya pembejeo za kilimo zinazowezesha ongezeko la mazao kama vile mbolea, mbegu na bidhaa za ulinzi wa mazao ya kilimo; vyakula vya mifugo na dawa za mifugo kwa ajili ya mifugo miongoni mwa suala mengine.

"Mbolea huongeza mazao. Kwa vile mimea hutumia virutubishi vilivyo kwenye udongo, tunavirejesha virutubishi hivyo kwa kutumia mbolea lakini wakulima hawana ufahamu wa maarifa ya kuweka vipimo sawa vya mbolea kulingana na mahitaji ya mimea," Grobbelaar alisema.

Usaidizi katika kilimo utakuza biashara ya chakula

Serikali ya Afrika Kusini inakuza maendeleo katika Sekta ya Wajasiriamali wadogo na wa kati (SME) na ukuaji wa wakulima wadogo wadogo ambao ni msingi mkuu katika kukumbana na suala la ukosefu wa usalama wa chakula nyumbani.

Kulingana na Ripoti ya Ufutiliaji wa Wajasiriamali wa Kimataifa (Global Entreprenuership Monitor Report- GEM) ya mwaka wa 2015/2016, licha ya mchango mkubwa wa Sekta ya Wajasiriamali wadogo na wa kati (SME) katika ukuaji wa kiuchumi na uundaji wa nafasi za ajira, biashara za Wajasiriamali wadogo na wa kati (SME) zinakumbwa na changamoto za ukosefu wa fedha miongoni mwa zingine. Ukosefu wa fedha ndio changamoto kuu kwa Wajasiriamali wadogo na wa kati (SME)- sekta ambayo inachangia katika asilimia 45 ya Jumla ya Pato la Kitaifa (GDP) la Afrika – Kusini – changamoto zingine ni kuacha biashara pamoja na ujuzi duni wa usimamizi wa biashaara ambao hutokana na ukosefu wa mafunzo na elimu ya kutosha.

Nchi ya Afrika Kusini inazalisha chakula cha kutosha na cha ziada kwa wananchi wake wote, lakini baadhi ya wananchi wa Afrika Kusini hawawezi kupata kiwango sahihi cha chakula na aina ya chakula kinachohitajika mwilini, ripoti hiyo ya mwaka wa 2014 iliyoandikwa na ya Maabara ya Chakula ya Afrika Kusini, shirika linalokuza usalama wa chakula katika eneo la Afrika Kusini inaeleza haya.

"Wanachi maskini wa Afrika Kusini hawawezi kutumia pesa kupata milo mbalimbali. Badala yake, chaguo lililopo la kuhakikisha kuna chakula na kupunguza njaa ni kulisha wanafamilia viwango vkubwa vya uji wa mahindi ambao hauna mahitaji yote ya virutubishi vinavyohitajika mwilini," haya ni kulingana na Laura Pereira, ambaye ni mwandishi wa ripoti hiyo.

Mwanzilishi wa Microsoft, Bill Gates, akizungumza kuhusu ukosefu wa uwekezaji katika sekta ya kilimo Barani Afrika, alisema kwamba uvumbuzi kutoka shambani hadi masoko ni mojawapo ya suluhu katika kubadilisha sekta ya kilimo-sekta ambayo inaajiri nusu ya jumla ya idadi ya watu barani Adfrika- ili biashara inawiri.

"Wakulima wa Afrika wanahitaji vifaa bora zaidi ili kuepuka majanga na kuwa na mazao ya ziada - mambo kama mbegu zinazoweza kuhimili ukame, mafuriko, wadudu, na ugonjwa, mbolea ya bei nafuu yenye mchanganyiko sawa wa virutubishi ili kuongeza virutubishi kwenye udongo," Gates alisema haya wakati aliwasilisha hotuba yake katika Mhadhara wa Nelson Mandela wa 14 mjini Pretoria, Afrika Kusini wiki iliyopita.

Gates alisema kwamba wakulima wanahitaji kuunganishwa na masoko ambapo wanaweza kununua pembejeo za kilimo, kuuza mazao yao ya ziada na kupata faida ili waweze kuiwekeza tena katika kilimo chao. Hiyo hatimaye itatoa fursa za ajira katika mashamba na sehemu zingine na kuunga mkono aina mbalimbai za biashara za kilimobiashara.